



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA JIJI LA TANGA



Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. CA/230/387/01

20 Desemba, 2024

Mkurugenzi,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania,
S.L.P. 938,
DAR ES SALAAM.

Yah: KIWANJA NA. 71 KITALU "A" NDAOYA AREA, JIJI LA TANGA

Tafadhali rejea somo tajwa hapo juu.

2. Ofisi yetu ilipokea ombi la Ardhi kiasi cha ekari 200 kwa ajili ya uwekezaji wa matumizi ya uhifadhi wa mafuta na gesi toka Kampuni ya kigeni ya **Pristine Berth Limited** katika eneo la Ndaoya, Jijini Tanga, ambapo baada ya ombi lao kukubaliwa, walilazimika kufanya utwaaji wa Ardhi hiyo kisheria na kisha kulipa fidia kwa wamiliki wa asili baada ya uthamini kufanyika na kuidhishwa na Mthamini Mkuu wa Serikali.
3. Baada ya ulipaji wa fidia kukamilika, ofisi yetu ilifanya upangaji na upimaji wa eneo hilo na kupatikana kiwanja Na. 71, Kitalu "A", Ndaoya Area, Jiji la Tanga, chenye ukubwa wa ekari 193.67 na kilichopimwa kwa ramani Na. E²/215/55 iliyosajiliwa kwa Na. 204281 tarehe 17.12.2024. Nakala ya ramani ya upimaji imeambatishwa na barua hii.
4. Kwa kuwa Kampuni hiyo ni ya Kigeni, napenda kuwasilisha kwako taarifa hizi kwa ajili ya hatua zako za utoaji wa cheti cha uwekezaji (*Certificate of Incentive*) kwa Kampuni husika ili taratibu za umilikishaji ziendelee.
5. Nakutakia kazi njema.

Eng. Juma Hamsini
MKURUGENZI WA JIJI

Nakala: Kamishna wa Ardhi Msaidizi
S.L.P 5058
TANGA

Mkurugenzi
Pristine Berth Limited
S.L.P. 78722
DAR ES SALAAM